**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18 NA MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

2. **Mheshimiwa Spika**, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na hivyo kuweza kukutana na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18. Mapendekezo ya Mpango ni ya mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya*

*Uchumi na Maendeleo ya Watu"*.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18, yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha hatua za maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti yatakayozingatiwa katika kukamilisha Mpango na Mwongozo ni pamoja na:

(i) Kushirikisha Sekta Binasi katika utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo;

(ii) Kuwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda kwa kupitia maendeleo ya viwanda vidogo vidogo – SIDO, kuboresha maeneo ya EPZA na SEZ;

(iii) Kuweka mfumo wa kulinda masoko ya bidhaa za ndani;

(iv) Kuchagua miradi michache ya kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti;
(v) Kukamilisha miradi ya maji na umwagiliaji kabla ya kuanza miradi mipya; na
(vi) Kuendelea na Mpango wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge.

4. **Mheshimiwa Spika,** kipekee nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Doto Mgosha James kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii na Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Aidha, tunawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo huu.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mhe. Kassim M. Majaliwa, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, na Watanzania wote kwa ujumla kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopatwa na

janga la tetemeko la ardhi lilitokea katika Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza na Mara Septemba 2016. Wapo wananchi waliopoteza maisha, waliojeruhiwa na kuharibikiwa na mali zao kutokana na janga hilo. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa waliojeruhiwa na wafiwa wote na kuwatakia afya njema.

6. **Mheshimiwa Spika,** pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliojitoa kwa hali na mali katika kuchangia wahanga wa tukio hilo. Ni heshima yangu kutambua michango ya Waheshimiwa Wabunge, Jumuiya ya Wafanyabiashara Nchini, Waheshimiwa Mabalozi, Wawakilishi wa Mashirika ya Umma na ya Kimataifa, Makampuni, Taasisi za Dini, Wafanyakazi wa Serikali, Watu Binafsi, Mashirika yasiyo ya Serikali, Vikundi Mbalimbali na Mtanzania mmoja mmoja. Michango hiyo imetumika na kuendelea kutumika kuleta nafuu kwa wahanga wa tukio hilo. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano na uzalendo wa hali ya juu walioonesha katika tukio hilo.

7. **Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa

mwaka 2017/18 yamezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015; Maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); na Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs)* sanjari na makubaliano ya kikanda, makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na makubaliano ya kimataifa yaliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SHABAHA NA MISINGI YA MPANGO NA BAJETI

8. **Mheshimiwa Spika,** katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/18 Serikali inatarajia kusimamia mambo muhimu kama ifuatavyo:

### Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla

9. **Mheshimiwa Spika,** shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha muda wa kati (2017/18 – 2019/20) ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2017, asilimia 7.9 mwaka 2018 na asilimia 8.2 mwaka 2019;

(ii) Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 5.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Kuwa na Pato ghafi la Taifa la Shilingi trilioni 123.9 mwaka 2017/18, Shilingi trilioni 139.7 mwaka 2018/19 na Shilingi trilioni 165.4 mwaka 2019/20;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18, asilimia 15.5 mwaka 2018/19 na asilimia 15.8 mwaka 2019/20;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 26.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18, asilimia 26.5 mwaka 2018/19 na asilimia 25.2 mwaka 2019/20;

(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 4.5 katika kipindi cha muda wa kati;

(vii) Kuwa na kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 15.0 mwaka 2017/18, asilimia 14.0 mwaka 2018/19 na asilimia 13.1 mwaka 2019/20;

(viii) Kuwa na nakisi katika urari wa malipo ya kawaida *(current account balance including transfers)* wa asilimia 6.3 ya Pato la Taifa katika kipindi cha muda wa kati; na

(ix) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4) katika kipindi cha muda wa kati.

**Misingi ya Mpango na Bajeti**

**10. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha muda wa kati (2017/18-2019/20), misingi ya mpango na bajeti ni pamoja na:

(i) Amani, usalama, utulivu na utangamano wa ndani na nchi jirani vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa;

(ii) Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, mfumuko wa bei, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika;

(iii) Uchumi wa Dunia kuendelea kuimarika na kutengemaa;

(iv) Bei za mafuta katika soko la Dunia hazitaongezeka;

(v) Hali ya hewa nchini na katika nchi jirani kuwa nzuri;

(vi) Mahusiano na nchi jirani, kikanda na kimataifa kuendelea kuwa mazuri; na

(vii) Kuwepo kwa sheria na taratibu wezeshi kwa uwekezaji.

## MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18

**11. Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kutoa maelezo kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18. Mapendekezo haya yanahusisha tathmini ya mwenendo wa uchumi na ustawi wa jamii, Hali ya Viwanda, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16 na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/18.

## TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

**12. Mheshimiwa Spika,** katika nusu ya kwanza (Januari hadi Juni) ya mwaka 2016, Pato ghafi la Taifa lilikuwa Shilingi trilioni 52.7 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 45.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Aidha, katika kipindi hicho ukuaji halisi

wa uchumi ulikuwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Shughuli zilizokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi hicho ni pamoja na: Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo (asilimia 17.4); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 13.7); Habari na Mawasiliano (asilimia 13.0); na Huduma za Fedha na Bima (asilimia 13.0). Shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo ni Huduma za Chakula na Malazi (asilimia 0.6) na Usambazaji Maji Safi na Udhibiti Maji Taka (asilimia 0.9). Ukuaji huu unajenga msingi wa kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2016.

**13. Mheshimiwa Spika**, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,918,928 sawa na Dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015. Tanzania inaendelea kuwa na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu ambapo inakadiriwa kuwa na watu milioni 50.1 mwaka 2016 na milioni 63 ifikapo mwaka 2025. Malengo ya Dira ya maendeleo ya Taifa ni kuwa na Pato la wastani la kila mtu la Dola za Kimarekani 3,000 ifikapo 2025. Hivyo, juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia malengo ya Dira ya kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

**14. Mheshimiwa Spika,** mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 6.5 Januari 2016 hadi asilimia 5.5 Juni 2016 na kupungua zaidi hadi asilimia 4.5 Septemba 2016. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na fedha, kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la Dunia hususan bei za mafuta ya petroli na kasi ndogo ya ongezeko la bei kwa bidhaa za chakula nchini. Matarajio ni kubaki na mfumuko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kwa kuongeza uzalishaji hususan wa chakula na kuimarisha sera za fedha na bajeti.

**15. Mheshimiwa Spika,** kiwango cha riba za amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 9.19 Julai 2015 hadi asilimia 9.97 Julai 2016. Aidha, kiwango cha riba za amana za mwaka mmoja kiliongezeka hadi asilimia 12.40 Julai 2016 kutoka asilimia 10.50 Julai 2015. Vile vile, wastani wa kiwango cha riba za mikopo kwa kipindi cha mwaka mmoja kilipungua kutoka asilimia 14.31 Julai 2015 hadi asilimia 13.31 Julai 2016. Tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.81 Julai 2015 na kufikia asilimia 0.9 Julai 2016. Mwenendo huu wa viwango vya riba

unaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara na ushindani nchini hivyo kuvutia zaidi uwekezaji wa Sekta Binafsi.

**16. Mheshimiwa Spika,** thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje katika kipindi kinachoishia Julai 2016 ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 9,810.4 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 9,128.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ilipungua kwa asilimia 18.3 kutoka Dola za Kimarekani milioni 13,569 Julai 2015 hadi Dola za Kimarekani milioni 11,003.4 Julai 2016 kufuatia kupungua kwa uagizaji wa bidhaa hususan bidhaa za ukuzaji mitaji na thamani ya mafuta. Kutokana na mwenendo huu wa uuzaji na uagizaji wa bidhaa nje, urari wa malipo ya kawaida uliimarika kutoka nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,778.9 Julai 2015 na kuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 1,866.1 Julai 2016.

**17. Mheshimiwa Mwenyekiti,** Akiba ya fedha za kigeni imebaki kuwa imara, ikiwa ni Dola za Marekani milioni 4,096.0 kufikia mwisho wa Septemba 2016, ambao ni uwezo wa kutosheleza

uagizaji nje wa bidhaa na hudumu kwa kipindi cha miezi 4. Kuongezeka (kutotetereka) kwa Akiba ya Fedha za Kigeni kunatokana na manunuzi yanayofanywa na Benki Kuu ya Tanzania kutoka kwenye soko la ndani la fedha za kigeni na mashirika ya umma.

**18. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2015/16, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilibaki kuwa imara hususan katika kipindi cha pili cha mwaka 2016/17. Kiwango cha ubadilishaji wa Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani kilipungua thamani kwa wastani wa asilimia 3.5 Juni, 2015, ambapo Juni 2016 kasi ya kupungua kwa thamani ilikuwa wastani wa asilimia 0.1. Kati ya Januari hadi Julai 2016 thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani ilishuka kwa kasi ndogo kutoka wastani wa Shilingi 2,172.38 kwa Dola moja Januari 2016 hadi wastani wa Shilingi 2,180.54 Julai 2016. Hali hii ilichangiwa na usimamizi madhubuti wa uchumi uliofanywa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, kupunguzwa kwa matumizi ya Serikali na kutoterereka kwa akiba ya fedha za kigeni.

**19. Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa (likijumuisha deni la ndani na nje) lilifikia Dola za Kimarekani milioni 18,614.93 sawa na ongezeko la asilimia 9.76 kufikia Juni 2016, ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 16,959.47 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya iliyochukuliwa kugharamia miradi ya maendeleo hususan ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, barabara na madaraja.

## UTEKELEZAJI WA WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2015/16

### Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**20. Mheshimiwa Spika,** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/16 ni pamoja na kukamilika kwa:

(i) Ujenzi wa km 382.9 za barabara kuu na ukarabati wa km 82.4 kwa kiwango cha lami;

(ii) Ujenzi wa madaraja ya Kigamboni, Maligisu, Nangoo, Mbutu na Ruhekei katika barabara kuu;

(iii) Ujenzi wa barabara na miundombinu ya mabasi ya mwendo kasi katika Jiji la Dar es Salaam (BRT Phase I, km 20.9) na huduma

zinatolewa kwa wananchi kuanzia Mei 2016;

(iv) Awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (km 25,954) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara;

(v) Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (km 542) na ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo;

(vi) Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi;

(vii) Usimikaji wa mitambo minne (4) ya kufua umeme Kinyerezi I yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 na kuanza uzalishaji wa umeme;

(viii) Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA Turnkey Phase II) na hivyo kuunganisha wateja 61,023 wa awali kati ya wateja 250,000;

(ix) Ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Iramba – Majita, Msangamkuu – Msemo, Ilagala – Kajeje, Igogo na Swea – Mwanza na ujenzi wa maegesho ya muda katika eneo la Magogoni - Dar es Salaam na Mbegani - Bagamoyo;

(x) Mradi wa Maji wa Ruvu Chini (Pwani); ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa km 55.3 kutoka kwenye mtambo Ruvu juu hadi matenki ya Chuo Kikuu cha Ardhi – Dar es Salaam;

upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu pamoja na ulazaji wa mabomba kutoka Mlandizi hadi Kimara; Miradi mipya 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148; uchimbaji visima 11 mkoani Tabora; upanuzi wa huduma ya maji safi katika manispaa ya Dodoma na mji wa Singida;

(xi) Ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kiwanda cha Viuadudu Kibaha - Pwani na ujenzi wa barabara za kuingia kiwandani kwa kiwango cha lami (mita 400);

(xii) Kutoa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159. Kati ya wanafunzi hao, 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na Washirika wa Maendeleo;

(xiii) Kutoa mikopo na ruzuku kiasi cha Shilingi bilioni 467.43 kwa wanafunzi 124,243 wa elimu ya juu ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 101,129;

(xiv) Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za sekondari 264; na

(xv) Kukamilika kwa ujenzi wa chuo cha mafunzo

ya ufundi cha Wilaya ya Makete (Makete District Vocational Training Centre).

**21.** **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/16 yapo katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya Tano**).

**HALI YA VIWANDA**

**22.** **Mheshmiwa Spika**, kati ya mwaka 2005 na 2013, mauzo ya bidhaa Duniani yalikua kwa wastani wa asilimia 7.5. Biashara ya bidhaa Duniani ilikua na kufikia zaidi ya Dola za Kimarekani trilioni 17, ambapo asilimia 83.0 ilitokana na bidhaa za viwandani. Bidhaa za viwandani kwa nchi za viwanda ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 5.2 katika kipindi hicho na kufikia Dola za Kimarekani bilioni 8,929 mwaka 2013. Karibu asilimia 58 ya mauzo ya bidhaa za viwandani Duniani yalihusisha bidhaa zinazotumia teknolojia ya kati na juu kama vile mitambo ya kemikali na bidhaa zake, vifaa vya mawasiliano na magari.

**23. Mheshmiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya mwisho ya Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya Mwaka 2013, Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda (vikubwa na vidogo) 49,243 ambapo, viwanda vikubwa vilikuwa 1,322 (asilimia 2.7) na vidogo ni 47,921 (asilimia 97.3). Sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani (manufacturing) iliongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda 48,474 (asilimia 98.4) ikifuatiwa na uchimbaji madini na mawe 391 (asilimia 0.8). Aidha, shughuli nne (4) za uzalishaji zilichangia asilimia 52.8 ya idadi ya viwanda nchini ambavyo ni bidhaa za chakula, 19,696 (asilimia 40.0), bidhaa za nguo 13,392 (asilimia 27.2), samani 6,823 (asilimia 13.9) na bidhaa za chuma isipokuwa mitambo na vifaa 3,805 (asilimia 7.7). Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda (vikubwa na vidogo) ambapo kati ya viwanda vikubwa 1,322 ilikuwa na viwanda 389 (asilimia 29.4), ukifuatiwa na Manyara 167 (asilimia 12.6), Arusha 89 (asilimia 6.7) na Kilimanjaro 66 (asilimia 5.0). Idadi kubwa ya viwanda 41,919 (asilimia 85.1) ina wafanyakazi mmoja hadi wane (1 – 4) na viwanda vichache 6,002 (asilimia 12.2) vina wafanyakazi watano hadi tisa (5 - 9).

**24. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu hali ya viwanda Kimataifa na Kitaifa yapo katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya Tatu**)

## MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2017/18

**25. Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/18 yamezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/18 yamegawanyika kama ifuatavyo:-

### Miradi ya Kielelezo

**26. Mheshimiwa Spika,** Miradi hii ni mahsusi, kwa maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo yake katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango. Miradi hii itajumuisha:- Makaa ya Mawe Mchuchuma; Chuma Liganga; ujenzi wa Reli ya Kati kutoka Dar – Tabora - Kigoma (km 1,251) kwa *Standard Gauge* na matawi yake ya: Tabora – Isaka – Mwanza (km 379); Isaka – Rusumo (km 371); Kaliua – Mpanda - Karema (km 321); Keza – Ruvubu (km 36); na Uvinza -

Kilelema kuelekea Musongati (km 203); kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi mkoani Lindi; uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi mkoani Tanga, Bagamoyo, Kigoma, Ruvuma na Mtwara; uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini; kusomesha vijana katika stadi maalum (mafuta na gesi, uhandisi na huduma za afya); uanzishwaji wa mji wa Kilimo wa Mkulazi; ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu; ujenzi wa barabara za Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310) na Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 868.7).

**Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda**

**27. Mheshimiwa Spika,** miradi itakayozingatiwa ni pamoja na: mradi wa Magadi Soda (Bonde la Engaruka); Kufufua Kiwanda cha General Tyre; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO; uendelezaji wa maeneo ya viwanda vidogo – SIDO katika mikoa ya Morogoro, Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; Bandari kavu (Pwani) na mradi wa bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi bandari ya Tanga.

**Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Maendeleo ya Watu**

**28. Mheshimiwa Spika,** katika **Elimu na Mafunzo ya Ufundi** maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Elimu msingi bila malipo; kujenga na kukarabati miundombinu ikiwemo madarasa, maabara, umeme, vyoo na maji kwa ajili ya elimu ya awali, msingi na sekondari; kuhakikisha upatikanaji wa madawati na walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi na hisabati; ujenzi na ukarabati wa karakana za kuandaa wanafunzi kwa njia ya vitendo katika vyuo vya ufundi nchini; ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vya ufundi na ualimu; kupanua matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya elimu ya juu na ufundi nchini; na kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuongeza uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi.

**29. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Afya na Ustawi wa Jamii,** maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuboresha Hospitali za Rufaa na mikoa kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa; kuimarisha upatikanaji wa huduma za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali, vituo vya

afya na zahanati; kuongeza udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza; kuimarisha huduma za kinga na magonjwa yasiyoambukiza; kupunguza vifo vya watoto na kina mama vinavyotokana na uzazi; na kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa jamii hususan vijana.

**30. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **maji**, maeneo ya kipaumbele ni pamoja na kulinda, kuendeleza na kusimamia vyanzo vya maji nchini pamoja na kudhibiti ubora wa maji; kuboresha usambazaji wa maji katika miradi ya kitaifa, makao makuu ya wilaya na miji midogo; kuboresha uwezo wa usambazaji wa maji safi na udhibiti wa maji taka na usafi wa mazingira; kupanua usambazaji wa maji vijijini; kuboresha usambazaji wa maji Dar es Salaam; na kujenga mabwawa katika mikoa yenye ukame pamoja na mkoa wa Dar es Salaam.

**Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji**

**31. Mheshimiwa Spika,** maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuendelea na miradi iliyoanza kutekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2016/17, ikiwa ni pamoja na: nishati; kilimo cha mazao; mifugo; uvuvi;

maji; umwagiliaji; miundombinu ya reli na barabara; ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara za jiji la Dar es Salaam; madaraja; bandari; kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga; usafiri wa majini; na miundombinu ya TEHAMA.

**Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**32. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kutekeleza miradi chini ya utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa kufua umeme Kinyerezi III MW 300; mradi wa mabasi ya mwendokasi Dar es Salaam awamu ya II, III na IV zenye jumla ya km 60; kiwanda cha kuzalisha madawa muhimu na vifaa tiba na mradi wa barabara ya tozo Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200).

**Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa**

**33. Mheshimiwa Spika,** maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma; miradi katika maeneo ya wanyamapori; misitu; mazingira na mabadiliko ya tabianchi; ardhi, nyumba

na makazi; madini; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; utawala bora na utawala wa sheria; kuwezesha uanzishwaji wa kanzidata ya miradi ya maendeleo katika ngazi zote; na kujenga uwezo katika idara zinazohusika na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

## MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18

**34. Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitoe maelezo kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18. Mwongozo huo unawaelekeza Maafisa Masuuli masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mipango na bajeti za mafungu yao. Maelekezo ya Mwongozo yanajumuisha utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; usimamizi na udhibiti wa matumizi; ulipaji na uzuiaji wa ongezeko la madeni ya Serikali; ukusanyaji wa mapato; mfumo wa bajeti wa mwaka 2017/18; na mfumo wa utoaji taarifa za utekelezaji. Aidha, Mwongozo unatoa mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/18.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO KWA MWAKA 2015/16

**35. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 Serikali iliandaa na **k**utekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali yaliyotolewa kwenye mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali. Maelekezo hayo ni pamoja na: kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima; kudhibiti ongezeko la madeni; na kusimamia ununuzi wa umma ili kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika.

**36. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa maelekezo hayo umewezesha kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia Shilingi trilioni 14.139 sawa asilimia 101 ya lengo la Shilingi trilioni 13.998. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi yalikuwa Shilingi trilioni 12.525 sawa na asilimia 101.3; mapato yasiyo ya kodi yalikuwa Shilingi trilioni 1.188 sawa na asilimia 106.8; na mapato ya halmashauri yalikuwa Shilingi bilioni 425.9 sawa na asilimia 81.6. Mafanikio hayo yalitokana na Maafisa Masuuli kuzingatia maelekezo ya kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato, kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usimamizi wa mashirika

yanayotoa michango na gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

**37. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 Maafisa Masuuli walizingatia maelekezo ya Mwongozo katika kudhibiti matumizi kwa: kupunguza safari za nje zisizo za lazima na maadhimisho ya sherehe mbalimbali; kufanya mikutano katika kumbi za Serikali; na kudhibiti posho zisizokuwa za lazima. Aidha, fedha zilizopatikana kutokana na hatua hizo zilitumika katika shughuli mbalimbali zikiwemo ujenzi wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi (Morocco – Mwenge, km 4.3) na barabara ya Mwanza (Ghana Quarters – Airport, km 9.15); ununuzi wa vitanda kwa ajili ya Hospitali ya Taifa Muhimbili; ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI; na ununuzi wa madawati kwa ajili ya shule za msingi ambapo pia wadau na wananchi wamechangia juhudi za Serikali. Utekelezaji wa hatua zilizoainishwa katika Mwongozo kwa mwaka 2015/16 uliwezesha Serikali kutekeleza majukumu ya msingi na hivyo kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/16 NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

**38. Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizojitokeza ni pamoja na: uwezo wa kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi kwenye mipaka ya nchi; kuendelea kukua kwa sekta isiyo rasmi na ugumu wa kukusanya kodi; kupatikana kwa wakati kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nje; mahitaji makubwa yasiyowiana na mapato; kuongezeka kwa madeni ya ndani; kubadilika kwa masharti na sera za upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi kutokana na mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara.

**39. Mheshimiwa Spika**, mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na: kuimarisha doria na upelelezi katika mipaka, bandari na bandari bubu kupitia Kikosi Kazi cha Kuzuia Magendo; kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuzuia mianya ya ukwepaji kodi; kuhakiki madeni na kutekeleza mkakati wa kuyalipa; kuendelea na jitihada za kurasimisha sekta isiyo rasmi; kurahisisha masharti

ya leseni za biashara na uwekezaji nchini; kuendelea kuimarisha soko la ndani la hati fungani za Serikali ili kuvutia ushiriki wa wawekezaji wengi; kukamilisha zoezi la kufanyiwa tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa; kufanya mapitio ya mkakati wa pamoja wa misaada na kuandaa mpango mpya wa mahusiano na washirika wa maendeleo; na kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji ili kuchochea uwekezaji kwa Sekta Binafsi.

## MWONGOZO WA MWAKA 2017/18

**40. Mheshimiwa Spika**, Mwongozo wa Mwaka 2017/18 ni mwendelezo wa utekelezaji wa maelekezo ya msingi yaliyotolewa na Serikali katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17. Baadhi ya maelekezo hayo ni pamoja na: mapato yote kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo kufuta utaratibu wa '*Retention*'; kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na kudai stakabadhi kwa bidhaa na huduma zilizotolewa; ukusanyaji wa kodi ya majengo kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; kutumia Taasisi za Umma katika huduma za bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (courier), matangazo na usafiri; kuhakiki watumishi

wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili; ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja/wingi (*in bulk*) kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji ili kupata nafuu ya bei; kutenga bajeti na kulipa michango ya Serikali katika mashirika ya kimataifa na kikanda kupitia Hazina; kufanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma; na kugharamia uendeshaji wa elimu msingi bila malipo kuanzia Januari 2016.

## MFUMO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18

**41. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2017/18, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi trilioni 32.946 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Hata hivyo, kiasi hiki ni makisio ya awali ambapo makisio ya mwisho yatapatikana baada ya kukamilika kwa tathmini ya nusu mwaka, 2016/17 pamoja na taarifa ya Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi kinachojumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

**42. Mheshimiwa Spika**, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Shilingi trilioni 20.872 sawa na asilimia 63 ya mahitaji yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya Shilingi trilioni 18.097 sawa na asilimia 87 ya mapato ya ndani. Mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 2.022 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni Shilingi bilioni 753.3. Serikali inategemea kukopa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 900 sawa na Shilingi trilioni 2.080 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara na Shilingi trilioni 4.434 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva. Aidha, Shilingi trilioni 1.859 sawa na asilimia 1.5 ya Pato la Taifa, ni mikopo mipya ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vile vile, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi trilioni 3.700. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 496.3 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti *(GBS)*, Shilingi trilioni 2.821 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 382.4 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta.

**43. Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya kina ya Sura ya Bajeti 2017/18 yapo katika Mwongozo wa

Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya nne, Jedwali Na. 4.1**).

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2017/18 Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi trilioni 32.946 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 19.782 zitatengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi trilioni 7.206 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma na Shilingi trilioni 9.723 kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa lililoiva. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi trilioni 13.164, sawa na asilimia 40 ya bajeti yote, ambapo fedha za ndani ni Shilingi trilioni 9.960 sawa na asilimia 76. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.343 ikilinganishwa na mwaka 2016/17.

## MAELEKEZO YA MWONGOZO KWA MWAKA 2017/18

### Maboresho ya Mfumo wa Kibajeti

**45. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika mfumo wa kibajeti ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi. Maboresho makubwa yaliyofanyika ni pamoja na kuandaliwa na

kupitishwa kwa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Hivyo, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuendelea kuzingatia Sheria ya Bajeti pamoja na Kanuni yake wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mipango na Bajeti.

**46. Mheshimiwa Spika,** Serikali imedhamiria kuandaa bajeti kwa kuzingatia Programu *(Programme Based Budget - PBB)* ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa umma. Mabadiliko haya yanatokana na maboresho mbalimbali yanayofanyika katika taasisi za kimataifa zinazosimamia masuala ya bajeti na fedha za umma. Mfumo huu utaanza kwa hatua ya majaribio katika Wizara nane (8) ambazo ni: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; na Wizara ya Nishati na Madini. Mfumo huu unawataka Maafisa Masuuli wa Wizara za majaribio kuainisha bajeti zao kwa utaratibu wa programu na kwa kuzingatia miongozo na viwango

vya kimataifa. Aidha, Maafisa Masuuli wa mafungu haya wanatakiwa kuandaa bajeti kivuli za mafungu yao kwa kuzingatia malengo ambayo yataonesha matokeo na viashiria vya kiutendaji vitakavyotumika kupima matokeo ya utekelezaji wa programu hizo.

**47. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015 Serikali ilitoa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma ambapo mafunzo ya mwongozo huo kwa watendaji wa mafungu mbalimbali yamefanyika mwaka 2016. Mwongozo huo, unatoa maelekezo mbalimbali ikiwemo: uibuaji na uchambuzi; ugharamiaji; utekelezaji; usimamizi; ufuatiliaji na tathmini; pamoja na usimamizi wa kanzidata ya miradi ya uwekezaji wa umma. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Mwongozo huo na kuhakikisha wanajenga uwezo wa wataalam kulingana na mahitaji ya mafungu yao.

**Uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18**

**48. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinaelekeza kuundwa kwa Kamati za Bajeti katika Serikali na taasisi zake ili kurahisisha maandalizi ya mipango na bajeti. Kamati za Bajeti zinaelekezwa kutekeleza majukumu yao katika uandaaji wa mipango na bajeti

kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Aidha, Maafisa Masuuli wa Taasisi na Wakala wa Serikali wanaelekezwa kuzingatia Nyaraka za Msajili wa Hazina katika uandaaji wa mipango na bajeti zao.

**49. Mheshimiwa Spika,** Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa Mipango na Bajeti ya Muda wa Kati *(MTEF)* na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya tatu ya Februari, 2017 kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha makadirio yao Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) wiki ya kwanza ya Februari, 2017 baada ya kupitishwa na Mamlaka husika na baadaye kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha rasimu ya mipango na bajeti katika Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma SURA 105.

**50. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya majumuisho ya bajeti za Mafungu na kuwasilisha kwenye ngazi za maamuzi za Serikali. Aidha, Mafungu yataandaa Randama za bajeti zao na kuwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta wiki ya tatu ya Machi, 2017 na wiki ya kwanza ya Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa Bungeni. Majumuisho ya bajeti yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kuanzia wiki ya pili ya Aprili, 2017 hadi wiki ya nne ya Juni, 2017. Utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya mwaka 2017/18 utaanza tarehe 1 Julai, 2017 hadi tarehe 30 Juni, 2018.

**51. Mheshimiwa Spika,** kuhusu kuhamisha shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujumuisha mahitaji ya kuhamia Dodoma katika mipango na bajeti kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa na Serikali. Mipango ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya Serikali iliyopangwa kujengwa Dar es salaam ihamishiwe Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo na miundombinu yoyote inayotegemewa kujengwa Dodoma ni lazima upate idhini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

**52. Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa utafanywa kwa pamoja baina ya Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Msajili wa Hazina na wadau wengine. Taasisi zote za Serikali zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha mipango na bajeti zao Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi kwa mujibu wa Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala tano (5) ngumu na laini za rasimu ya mipango na bajeti zao kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalamu. Vile vile, zinapaswa kuwasilisha nakala tatu (3) za mipango na bajeti iliyosainiwa kwa mamlaka husika. Mikoa na Halmashauri zinapaswa kuwasilisha nakala tatu (3) za *MTEF* zilizosainiwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pia, Taasisi za Umma zinatakiwa kuandaa na kuwasilisha mipango na

bajeti na kuwasilisha nakala tatu (3) zilizosainiwa kwa Wizara zinazoratibu bajeti zao na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ili kuweka ufafanuzi na uwazi katika zoezi la uchambuzi wa bajeti, majadiliano yataendeshwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16;

(ii) Kupitia mapato na matumizi ya kipindi cha nusu mwaka wa 2016/17, changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo;

(iii) Kanuni za uandaaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/18 *(MTEF)* kama ilivyoelekezwa katika Sura ya Tano ya Kiambatisho cha Mwongozo;

(iv) Vipaumbele vilivyotolewa katika Mwongozo na ukomo wa bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(v) Kuwasilisha mipango na bajeti iliyoandaliwa kwa Mfumo wa Utengaji Bajeti wa Kimkakati *(Strategic Budget Allocation System – SBAS)* kwa upande wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na *PlanRep* kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015; na

(vii) Maelekezo ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni yake ya mwaka 2015, Nyaraka za Msajili wa Hazina, pamoja na Nyaraka na Miongozo mingine ya Serikali.

**54. Mheshimiwa Spika,** kuhusu uingizaji wa takwimu za bajeti katika Mfumo wa Malipo *(IFMS),* kulingana na ratiba ya maandalizi na uchambuzi wa bajeti, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kukamilisha kwa wakati zoezi la kuingiza takwimu za bajeti kwenye mfumo wa malipo na kuhakikisha usahihi wa takwimu hizo;

(ii) Kuzingatia Mfumo wa Kimataifa wa mwaka 2014 wa Takwimu za Kifedha za Serikali *(GFS Codes)* toleo la mwaka 2014 na za miradi *(Project Codes)* kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(iii) Kutumia vizio vilivyokubalika na vinavyotolewa katika mfumo wa *SBAS* na *PlanRep*; na

(iv) Kuweka makadirio sahihi ya gharama za kodi ya pango, umeme, maji na simu.

## MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

**55. Mheshimiwa Spika,** viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa vitatolewa kwa kuzingatia vigezo vya ugawaji rasilimali na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo huu. Aidha, hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vitakavyotolewa. Kwa msingi huo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia ukomo wa viwango vya bajeti vilivyoidhinishwa kwa mwaka 2017/18.

**56. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeandaa mikakati na hatua za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kama ilivyoainishwa katika Sura ya Nne ya Kiambatisho cha Mwongozo huu. Jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali ni la Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakusanya mapato kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango na kuwasilisha kwenye

Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti zitakazoidhinishwa katika mafungu yao. Vile vile, Taasisi na Wakala za Serikali zinaelekezwa kuendelea na akaunti zao za mapato zilizopo Benki Kuu ya Tanzania na kuwa na akaunti ya matumizi katika benki za biashara. Ili kutimiza lengo hili, Taasisi na Wakala zote zinatakiwa kuwasilisha mapato yote katika akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania ndani ya saa 24 baada ya kukusanywa.

**57.** **Mheshimiwa Spika**, mgao wa fedha kutoka akaunti za mapato zilizo Benki Kuu ya Tanzania kwenda kwenye akaunti za matumizi za Taasisi zilizo katika benki za biashara utazingatia Mpango wa Mtiririko wa Fedha wa bajeti iliyoidhinishwa. Fedha kwa ajili ya matumizi ya Taasisi na Wakala za Serikali zitasimamiwa na Msajili wa Hazina kulingana na Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha na bajeti iliyoidhinishwa.

**58.** **Mheshimiwa Spika**, Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuweka mazingira wezeshi katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji

wa mapato;

(ii) Kuhakikisha kuwa majengo yote yanathaminishwa kulingana na bei halisi ya soko. Aidha, majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa viwango vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Zoezi hili lifanyike kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo likikamilishwa;

(iii) Kupima na kuainisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati miliki ya ardhi;

(iv) Urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi;

(v) Kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(vi) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(vii) Kuingia mikataba na wazabuni, makandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za *EFD*;

(viii) Kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya;

(ix) Kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango; na

(x) Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vituo vya ukusanyaji wa mapato kama vile bandari, viwanja vya ndege na mipakani.

**59. Mheshimiwa Spika,** Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa utaratibu wa kupata mikopo kwa miradi mipya na inayoendelea uzingatie Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, mapitio ya mkopo yatazingatia Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, SURA 290. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kupata idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango kabla ya kukopa kama ilivyobainishwa katika Kifungu Na. 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

**60. Mheshimiwa Spika,** kuhusu ulimbikizaji wa madeni ya ndani, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia Kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Waraka Na. 4 wa

Mwaka 2014 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni. Kutokana na hali hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa;
(ii) Kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa;
(iii) Kubainisha madeni yaliyopo na kuhakikisha yanaingizwa kwenye hesabu za majumuisho za Serikali;
(iv) Kuingiza matumizi yote kwenye Mfumo wa Malipo wa IFMS; na
(v) Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na kuingizwa kwenye hesabu za fungu husika (*Financial Statement*).

**61. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kudhibiti madeni sanjari *(contingent liability)* hususan yenye dhamana ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mikataba inayoweza kusababisha madeni. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia madeni sanjari yote katika maandalizi ya bajeti zao.

**62. Mheshimiwa Spika,** kuhusu kudhibiti matumizi, Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo bila kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa:

(i) Kuhakikisha mikataba inayoingiwa na Serikali na taasisi zake inakuwa katika Shilingi za Kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara za kimataifa;

(ii) Kuendelea kupunguza gharama na matumizi yasiyokuwa ya lazima ikiwemo sherehe za kitaifa, posho za vikao, uchapishaji wa fulana, kofia, mikoba, safari za nje, mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na ununuzi wa samani kutoka nje;

(iii) Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo, warsha na semina inafanyika katika kumbi za Serikali na Taasisi za Umma;

(iv) Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma na zile ambazo Serikali inamiliki hisa katika kununua huduma kama vile bima, huduma za fedha, usafirishaji wa barua, wavuti, simu, mizigo na vifurushi, matangazo na usafiri. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia unafuu na ubora wa huduma zinazotolewa na taasisi hizo;

(v) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoundwa

kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali;

(vi) Kudhibiti ununuzi wa bidhaa, huduma na ujenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha ya ununuzi inapatikana kwa kutumia utaratibu wa *Force account,* ununuzi wa bidhaa ya pamoja/wingi, ushindani na kupitia masoko ya ndani;

(vii) Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipia ankara hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa;

(viii) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo ya umeme, maji na simu ili kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

(ix) Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili pekee;

(x) Kutumia utaratibu wa ununuzi wa nyumba kwa utaratibu wa kulipia kwa awamu (mortgage financing arrangement) hususan kwa majengo ya balozi na wawakilishi walioko nje ya nchi badala ya utaratibu wa kupanga;

(xi) Kudhibiti safari za nje ya nchi na ukubwa wa

misafara;

(xii) Kuhakikisha ununuzi wa magari unafanyika kwa pamoja kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (*GPSA*) baada ya kupata kibali cha ununuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(xiii) Kuthibiti utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi waliokidhi vigezo pekee ndio wananufaika na mikopo hiyo; na

(xiv) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufanikisha mawasiliano katika Ofisi za Serikali, hususan katika kipindi cha mpito cha Serikali kuhamishia shughuli za Makao Makuu Dodoma.

**63. Mheshimiwa Spika,** Maafisa Masuuli wanapaswa kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti ya mwaka 2017/18 na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika ipasavyo. Ili kufanikisha lengo hili, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinasisitizwa kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele kwenye masuala mtambuka. Vipaumbele hivyo ni pamoja na masuala ya kijinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi

pamoja na mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kuweka kipaumbele katika masuala yote yanayohusu watu wenye mahitaji maalum hususan ajira, afya, elimu, na ujenzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

**64. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kutekeleza maboresho ya masuala mtambuka ambayo ni ya muhimu katika utawala bora, uboreshaji wa huduma na uwajibikaji. Maboresho haya yanajumuisha: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma *(PSRP)*, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa *(LGRP)*, Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria *(LSRP)*, Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(PFMRP)*, Maboresho ya Sekta ya Fedha *(SGFRP)*, Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara *(BEST)*, na Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Rushwa *(NACSAP)*. Maboresho mengine ya kuzingatia ni pamoja na Udhibiti wa Fedha Haramu, Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi, Mfumo wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini zenyewe *(APRM)*, na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu. Hivyo, kila taasisi inapaswa kuzingatia majukumu yake na

kuhakikisha inatenga fedha za kutekeleza kwa ukamilifu maboresho yanayozihusu.

**65. Mheshimiwa Spika,** katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali itaendelea kutenga Shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kupitia Mfuko ambao utakuwa wa Mzunguko *(Revolving Fund)*. Mfuko huo utasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kutekelezwa na Halmashauri za Wilaya. Katika ngazi ya kijiji, Mfuko utasimamiwa na Kamati ya Mfuko ya Kijiji. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia kuwa miradi/biashara itakayofaidika inachaguliwa kwa kuzingatia vigezo na masharti ya Mfuko.

**66. Mheshimiwa Spika,** kuhusu usimamizi wa mali za umma, Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi wa mali za umma zilizo chini ya sekta zao. Aidha, wanapaswa kupanga na kutenga fedha za kuhakiki, kupima, kuweka mipaka na kurasimisha umiliki wa mali za umma kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji taarifa. Mali hizo ni pamoja na viwanja vya Serikali, maeneo ya wazi, viwanda, shule, vyuo vikuu, hospitali, vituo vya afya, zahanati, jeshi na vyombo vya usalama na mashamba ya umma.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Halmashauri wanapaswa kuwezesha umiliki wa mali hizo.

**67. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutekeleza miradi katika utaratibu wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)*. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sheria ya *PPP* Na. 18 ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Ili kukuza utekelezaji wa miradi ya *PPP,* vipaumbele vitatolewa kwa miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinatakiwa kukamilisha upembuzi yakinifu ili kuwezesha miradi hiyo kupitia mfumo wa *PPP*. Katika kuanzisha miradi ya *PPP* na kujenga uwezo wa kitaasisi, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye Mfuko wa Uwezeshaji wa *PPP*.

**68. Mheshimiwa Spika,** kuhusu maelekezo mahsusi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika **Aya Na. 52** ya Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya

Serikali kwa Mwaka 2017/18.

## UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

**69. Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji na tathmini utafanyika ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utekelezaji kulingana na thamani halisi ya fedha za umma zinazotumika. Kwa msingi huu Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo, programu na shughuli zote za Serikali zinabuniwa vizuri, kupangwa kwa mtiririko na kutenga fedha kwa kuzingatia mipango na bajeti iliyoidhinishwa.

**70. Mheshimiwa Spika,** taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (kwa Taasisi za Umma) zikiwa katika nakala ngumu na laini. Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuwasilisha taarifa hizo kwa mujibu wa muundo uliooneshwa katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

**HITIMISHO**

**71. Mheshimiwa Spika,** Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

**72. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wadau wote na wananchi wanaoendelea kuchangia masuala mbalimbali ya mipango na bajeti ya Serikali. Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha za kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwezesha ushiriki mkubwa zaidi wa Sekta Binafsi na wananchi hususan katika maeneo ambayo yatakuza viwanda na maendeleo ya watu nchini.

**73. Mheshimiwa Spika,** hotuba hii pamoja na vitabu vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz) na Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz).

74. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kutoa maoni na kushauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

75. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.